

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**621**

**KISWAHILI**

**Muda: Saa 3**

**Jumatatu, 04 Mei 2015 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **wawili** (2) kutoka sehemu B na maswali **mawili** (2) kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B na C zina alama 30 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwa** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## **SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha sehemu kuu nne katika utungaji wa Kiswahili.
2. Eleza kwa ufupi matumizi manne ya alama za majaribio ya somo la Kiswahili.
3. (a) Toa sababu mbili za umuhimu wa wanafunzi kujifunza kusoma kwa sauti katika shule za msingi.  
(b) Taja aina mbili za kusoma.
4. Eleza kwa kifupi faida nne za njia shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji.
5. Ainisha sifa nne za lugha.
6. Eleza kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya kitabu cha kiada na muhtasari.
7. (a) Ainisha makundi mawili ya stadi za lugha.  
(b) Taja aina mbili za utungaji.
8. Eleza kwa kifupi madhumuni manne ya kufundisha Kiswahili katika shule za msingi.
9. Bainisha aina nne za barua.
10. Bainisha njia nne shirikishi zinazoweza kutumika kufundishia na kujifunzia Kiswahili.

## **SEHEMU B (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

11. Eleza kwa mifano faida tano tunazopata kutohana na kutumia kamusi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.
12. Huku ukitoa mifano kwa kila kimoja, eleza jinsi viungo vifuatavyo vinavyohusika katika kuzungumza.
  - (a) Ulimi
  - (b) Ufizi
  - (c) Kidakatonge
  - (d) Kaakaa laini
  - (e) Kaakaa gumu.

13. Andika insha yenyе jumla ya maneno 300 juu ya "UMUHIMU WA KUTUNZA MAZINGIRA".
14. Fafanua aina tano za maneno ya Kiswahili huku ukitoa mfano wa sentensi moja kwa kila aina ya neno.

### **SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii.

15. Eleza njia tano utakazotumia kufundisha msamiatи kwa wanafunzi wa Darasa la Tano.
16. Fafanua aina nne za tathmini zinazoweza kutumika somo la Kiswahili.
17. Eleza sababu tano zinazoonesha umuhimu wa mwalimu wa somo la Kiswahili kufanya masahihisho darasani baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi.
18. Fafanua mambo manne yanayosababisha kubadilika kwa muhtasari na vitabu vya kufundishia na kujifunzia katika somo la Kiswahili.